JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
OFISI YA WAZIRI MKUU
TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA

HALMASHAURI YA WILAYA YA MPWAPWA

# SHULE YA SEKONDARI KIMAGHAI "A".

JINA LA MWANAFUNZI ………………….……………………………………………

**YAH: MAAGIZO YA KUJIUNGA NA KIDATO CHA TANO KATIKA SHULE YA SEKONDARI KIMAGHAI "A" MWAKA ...............................**

**P O N G E Z I  N A  K A R I B U** Kwa niaba ya jamii nzima ya Shule ya Sekondari ya Kimaghai A, nakupongeza sana kwa kuchaguliwa kujiunga na shule yetu Kwa tahasusi ya ........................ Kwa pamoja tunakukaribisha sana. Yafuatayo ni maagizo ya kujiunga na shule hii.

1.0 Mwanafunzi anatakiwa kufika shuleni kuanzia tarehe 05/07/2026 hadi tarehe 14/07/2026.

**2.0 NAMNA YA KUFIKA SHULENI.**

Shule yetu ipo Mkoa wa **Dodoma**, Wilaya ya **Mpwapwa**, kata ya **Kimagai** kutoka Mpwapwa mjini mpaka kata ya kimagai kunaumbari wa km 16.kutoka stendi ya mpwapwa Mjini kuna usafiri wa magari mpaka kimagai kwa nauri ya tsh 2,000.kutoka stendi ya kata ya kimagai hadi shule ilipo kuna umbali wa km 1 ambapo unaweza kutembea kwa mguu au kwa bodaboda tsh 1,000.Mji wa Mpwapwa una umbali wa kilometa 120 kutoka Dodoma Mjini na unafikika kwa mabasi ya moja kwa moja kutoka Dodoma. Upo usafiri wa kila siku wa mabasi kutoka Dodoma ambayo hufanya safari zake kuanzia saa 03:00 asubuhi hadi saa 11:00 jioni. (Nauli Sh. 8,000/=) Usipopata usafiri wa aina hii unaweza kupanda mabasi yanayoelekea Gairo, Morogoro au Dar Es Salaam na kushuka kituo cha ***Mbande***, mahali ambapo ni njia panda ya kuelekea Mpwapwa na Kongwa. Tafadhali sana usipande gari au basi linaloekea Kongwa, subiri gari linaloelekea Mpwapwa.

Endapo unatokea Dar-es-Salaam au Morogoro unashauriwa kutumia basi lolote kati ya mabasi yanayofanya safari zake kuja Mpwapwa moja kwa moja; usafiri huu upo kila siku. Ukikosa basi la moja kwa moja tumia basi lolote linaloelekea Dodoma na uteremkie Mbande na kupata usafiri wowote unaolekea Mpwapwa. Unatahadharishwa tena kutotumia magari yanayoishia Kongwa.

Kwa wale watakaotumia usafiri wa treni, tunashauri kuteremkia Dodoma mjini ambapo ni rahisi kupata usafiri wa kuelekea Mpwapwa Mjini moja kwa moja. Mabasi yanayokuja mpwapwa huanzia safari zake Dodoma Mjini kwenye kituo kiitwacho ***Soko la Ndugai lililopo karibu na stendi kuu ya mkoa eneo la Nanenane.***

3.0 **MAMBO MUHIMU YA KUZINGATIA**

i. **Sare ya shule:**

ii. **WAVULANA:**

Mashati meupe mawili (2) ya tetroni ya mikono mirefu, suruali mbili (2) za heshima zenye marinda za rangi ya dark blue (siyo za kubana na chini iwe na upana wa inchi 16 pia iwe na mkunjo wa chini) ,viatu vyeusi vya kufunga kwa kamba (vya kupigwa na kiwi) na tai ndefu ya dark blue na soksi nyeusi.

Wakati wa michezo wanafunzi watatumia fulana (tazama picha kama inavyoonekan a hapo chini)



**Sare zifuatazo mwanafunzi atazipata shuleni;**

i. **T-shirt zenye nembo ya shule(moja ya darasani kwa baadhi ya siku na mbili za kushindia (03)).**
ii. **Track suit yenye nembo ya shule.**
iii. **Sweta la darasani lenye nembo ya shule.**
iv. **Kizibao.**

Track suit itatumika wakati wa michezo na katika kufanya kazi za mikono. Shamba dress pia zitavaliwa baada ya chakula cha mchana na wakati wa usiku zitavaliwa na koti la track suit kujikinga na baridi.

**N.B** Jacketi halitaruhusiwa ndani ya eneo la shule.

iii. **WASICHANA;**

Mashati meupe mawili (2) ya tetroni ya mikono mirefu, sketi mbili(2)draft mshono wa rinda box (rinda pana nyuma na mbele) iwe ndefu mpaka kwenye kifundo cha mguu, viatu vyeusi vya kufunga kwa kamba (vya kupigwa na kiwi) na tai ndefu ya dark blue na soksi nyeupe.

(tazama picha ya kitambaa cha sketi kama kinavyo onekana hapo chini)



Wakati wa michezo wanafunzi watatumia fulana pamoja na tight ndefu nyeusi (tazama picha kama inavyoonekan a hapo chini)



**Sare zifuatazo mwanafunzi atazipata shuleni;**

a) **T-shirt zenye nembo ya shule(moja ya darasani kwa baadhi ya siku na mbili za kushindia (03)).**
b) **Track suit yenye nembo ya shule.**
c) **Sweta la darasani lenye nembo ya shule.**
d) **Kizibao.**

Track suit itatumika wakati wa michezo na katika kufanya kazi za mikono. Shamba dress pia zitavaliwa baada ya chakula cha mchana na wakati wa usiku zitavaliwa na koti la track suit kujikinga na baridi**.**

**N.B**

- Jacketi halitaruhusiwa ndani ya eneo la shule**.**
- Mwanafunzi anatakiwa kunyoa nywele **fupi**, saizi moja na sio mtindo wa panki ama kiduku lakini pia sio **kipara** (kutoa nywele zote kichwani).
- Wanafunzi wenye ulemavu wa ngozi (**ALBINO**) waje na mashati ya mikono mirefu pamoja na kofia za kujikinga na jua

**SARE BAADA YAMASOMO:**

Baada ya masomo wanafunzi wanatakiwa kuvaa sare maalumu (shamba dress); Suruali nyeusi za kitambaa zenye marinda-chini zenye upana wa inchi 16 na mkunjo wa chini (aje nazo mbili) zenye heshima na maadili ya kitanzania pamoja na na mkanda mweusi.
Kwa wasichana waje na sketi nyeusi (02) zenye marinda ya kawaida

**N.B VAZI LA HIJABU**: - Pamoja na maelekezo (i) – (x) vazi la Hijabu linaruhusiwa kwa kuzingatia: -

(i) Hijabu nyeupe kwa ajili ya darasani.
(ii) Hijabu ya nje ya darasa rangi ya maziwa.

**ZINGATIA.**

(i). Nguo ambazo siyo sare ya shule haziruhusiwi shuleni. Ukaguzi wa vifaa/vitu vyote vitakavyoletwa shuleni utafanyika. Ukipatikana na vifaa/nguo zisizohitajika utalazimika kuzirudisha nyumbani. Mwanafunzi aripoti shuleni akiwa amevaa sare mwanafunzi atayekuwa hajavaa sare za shule hatapokelewa.
(ii). Mwanafunzi hatakiwi kusuka wala kuwa na nywele ndefu, kucha ndefu, wala kupaka rangi kwenye kucha.

3.**2 VIFAA VINGINE AMBAVYO MWANAFUZI ANATAKIWA KUJA NAVYO MWANAFUNZI**.

i.) Madaftari makubwa (counter books) kumi (10)
ii.) Kalamu ya wino (pen,) penseli na rula.
iii.) Galoni au chombo kidogo cha kuhifadhia maji yakunywa.
iv.) Fedha kiasi (Pocket money) cha uwezo wako kwaajili ya mahitaji yake.
v.) Mkebe
iv) Scientific calculator.
v) Picha 04 (nne) za "Passport size" kwa matumizi ya ofisi.
vi) Raba na soksi ndefu (wavulana),tight ndefu nyeusi (wasichana) kwa ajili ya michezo.
vii) Tochi moja ya kusomea ya betri za kawaida ama ya kutumia nishati ya jua (solar) kwa ajili ya kusomea na kutumia wakati umeme unapokatika shuleni
viii) Vitabu vinavyoendana na Tahasusi yake.
ix) Bunda 02 (mbili A4) za karatasi (Ream) kwa mwaka.
x) Ndoo mbili (lita 10).
Viii) Godoro ukubwa wa 3x6 lenye foronya na mto mmoja.
ix) Shuka mbili rangi ya sky blue (wavulana) na rangi ya pink (wasichana).
x.) Chandarua nyeupe yenye ukubwa wa 3½
xi. ) Vyombo vya chakula ;Sahani, bakuli, kikombe (aina ya mfupa) kijiko na chupa ya maji ya kunywa.
xii.) Nguo za ndani za kutosha, taulo za kike, sabuni za kuogea na kufulia, miswaki na dawa ya meno, mafuta ya kupaka ya mgando.

xiii.) Kitenge au khanga pamoja na taulo, blanketi zito.
xiv.) Mwanafunzi haruhusiwi kuja na begi tofauti na Sanduku imara (trunker) na begi la darasani.

**VIFAA VYA USAFI.**

| | KIFAA | IDADI |
|---|---|---|
| 01 | Dawa ya chooni (ARO – toilet cleaner) | 02 PCS - HGK |
| 02 | Sabuni ya maji | Lita 05 (1 pc) - HGL |
| 03 | Ufagio wa ndani | 02 pc -HGL |
| 03 | Squizer | 02 pc - HGL |
| 05 | Fagio ngumu | 02 pc - HGK |
| 06 | Brush ndogo za chooni | 02 pc - HGKH |
| 07 | Reki | 01 pc - HGL |
| 08 | Jembe na mpini | 01 pc - HGK |
| 09 | Kwanja | 01 pc - HGK |
| 10 | Moper ( dekio lenye nyuzi) | 01 pc - HGK |
| 11 | Panga | 01 pc - HGL |

**ANGALIZO.**

a) Mwanafunzi asije na mizigo au begi kubwa shuleni, aje na Tranka moja tu.

a) Hairuhusiwi mwanafunzi kutembelewa na wageni wakati wote. Atakaokuwepo hapa shuleni isipokuwa kwa wito iwapo italazimika. Siku ya kuwaona wanafunzi ni siku ya kikao cha wazazi au mahafali.

b) Ni muhimu kwa mzazi/mlezi kutoa nafasi kwa walimu kufanya kazi zao bila

usumbufu kwa kumshirikisha mwanafunzi mambo yasiyo na tija kwake akiwa shuleni.
c) Mwanafunzi hatakiwi kutumia mafuta makali/ marashi (pefume) na kipodozi cha aina yoyote.

**4.0. MICHANGO YA UENDESHAJI WA SHULE.**

Michango ya shule kwa mwaka ni shilingi **80,000/=** kwa mwanafunzi wa bweni. Fedha hizo zilipwe kwenye akaunti ya shule NO. **50410029131 (KIMAGHAI A Secondary School Revenue Collection).** katika benki ya **NMB**. (Tafadhari andika majina kamili ya mwanafunzi kwenye stakabadhi ya malipo (pay in slip) hata kama ni mtu mwingine anamlipia) na kuja nayo shuleni.

5.0. **SHERIA NA KANUNI MUHIMU ZA KUZINGATIA MWANAFUNZI AWAPO SHULENI.**

Shule inaendeshwa kwa mujibu wa Sheria ya Elimu Na. 25 ya mwaka 1978 na kama ilivyo rekebishwa kwa Sheria Na. 10 ya mwaka 1995. Aidha, inazingatia miongozo yote inayotolewa na Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia yenye dhamana ya elimu na Ofisi ya Rais – TAMISEMI yenye jukumu la usimamizi na uendeshaji wa elimu nchini. Unatakiwa kuzingatia mambo ya msingi yafuatayo ambayo yanafafanuliwa kwa maandishi na utapewa nakala yake mara baada ya kuripoti shuleni. Mambo hayo ni pamoja na;

a) Heshima kwa viongozi, wazazi, wafanyakazi wote, wanafunzi wengine na jamii kwa ujumla ni jambo la lazima.
b) Mahudhurio mazuri katika kila shughuli ndani na nje ya shule kulingana na ratiba ya shule;
c) Kushiriki kwa kikamilifu masomo ya usiku na alfajili (Preparation);
d) Kuwahi katika kila shughuli za shule utakazopewa;
e) Kufahamu mipaka ya shule na kuzingatia kikamilifu maelekezo ya kuwepo ndani na nje ya shule ya mipaka hiyo wakati wote wa uanafunzi wako katika shule hii;
f) Kutunza usafi wa mwili, mavazi na mazingira ya shule;
g) Kuvaa sare ya shule wakati wote unapotakiwa;
h) Kuzingatia ratiba ya shule wakati wote;
i) Kutunza mali za shule;
j) Mwanafunzi haruhusiwi kubadili dini wala kumshawishi mwanafunzi mwenzake kubadili dini wawapo shuleni.
k)Ni marufuku mwanafunzi kumiliki vifaa vyenye ncha kali na dawa bila idhini ya daktari;

**MUHIMU:**

a) Mwanafunzi hapaswi kuja na simu shuleni kwa namna yoyote ile, na hakuna mtumishi anayeruhusiwa kutunza simu ya mwanafunzi pia;
b) Mwanafunzi awapo shuleni atatakiwa kulala kwenye Bweni alilopangiwa na kitanda alichopangiwa. Ni marufuku mwanafunzi kulala kitanda kimoja na mwenzake au kuishi kwenye Bweni ambalo hakupangiwa. Mwanafunzi ataruhusiwa kurudi nyumbani kwa ruhusa na kibali maalum toka kwa Mkuu wa Shule ( Ugonjwa au msiba wa baba, mama au ndugu wa tumbo moja.)

**6. 0 .Makosa yatakayosababisha Mwanafunzi kufukuzwa Shule ni pamoja na:**

a) Wizi;

b) Kutohudhuria masomo kwa zaidi ya siku 90 bila taarifa/utoro;

c) Kugoma na kuhamasisha mgomo;

d) Kutoa lugha chafu kwa wanafunzi wenzake, walimu/walezi na jamii kwa ujumla

e) Kupigana mwanafunzi kwa mwanafunzi, kumpiga mwalimu au mtu yeyote yule

f) Kufuga nywele na kucha

g) Ulevi au unywaji wa pombe na matumizi ya dawa za kulevya, Uvutaji wa sigara;

h) Uasherati, mahusiano ya jinsi moja, kuoa au kuolewa;

i) Kupata ujauzito au kutoa mimba;

j) Kushiriki matendo ya uhalifu, siasa na matendo yoyote yale yanayovunja sheria za nchi;

l) Kwenda kwenye nyumba za starehe na nyumba za kulala wageni;

m) Kumiliki, kukutwa au kutumia simu ya mkononi katika mazingira ya shule;

n) Kudharau Bendera ya Taifa;

o) Kufanya jaribio lolote la kujiua, au kutishia kujiua kama kunywa sumu;

p) Uharibifu wa mali ya umma kwa makusudi.

7.0 VIAMBATANISHO VYA FOMU MUHIMU

a) Barua ya utambulisho wa mwanafunzi na mzazi kutoka mamlaka ya Serikali ya mtaa anakotokea mwanafunzi zikiwa na picha za wahusika.

b) Fomu ya Uchunguzi wa Afya (Medical Examination Form) ambayo itajazwa na Mganga Mkuu wa Hospitali ya Serikali na apige mhuri wa ofisi yake; Fomu Na 03

c) Fomu ya Maelezo Binafsi kuhusu Mwanafunzi/Mkataba wa kutoshiriki katika migomo, fujo na makosa ya jinai na ahadi; Fomu Na 02

d) Fomu ya mzazi kukiri kukubaliana na sheria, kanuni na maelekezo mengine yanayotolewa na shule; Fomu Na 01.

**TAFADHALI SOMA KWA MAKINI MAELEKEZO/MAAGIZO HAYA KIKAMILIFU NA KUYATEKELEZA.**

KARIBU SANA KATIKA SHULE HII

**.................................**

**EUDIA JELEMIA MEDAA**

**MKUU WA SHULE**

**TAFADHALI UPATAPO UJUMBE WOWOTE KUHUSU MWANAFUNZI/MTOTO WAKO USITUME CHOCHOTE, NI VEMA UKAWASILIANA NA UONGOZI WA SHULE ILI KUPATA UKWELI WA TAARIFA.**

HUSIKA NA NAMBA ZIFUATAZO;

| | |
|---|---|
| MKUU WA SHULE | 06-20251277/07-62040211 |
| MAKAMU MKUU WA SHULE | 07-68212641/06-10132641 |
| MTAALUMA MWANDAMIZI | 06-18524454 |

**FOMU NA 01.**

**KIAPO CHA MWANAFUNZI.**

**OFISI YA WAZIRI MKUU**
**TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA**
**HALMASHAURI YA WILAYA YA MPWAPWA**
**SHULE YA SEKONDARI KIMAGHAI A**
**FOMU YA KUKUBALI SHULE**

**A. SEHEMU YA MWANAFUNZI.**

1. Mimi (majina kamili matatu) ................................................................. .
   Nimekubali kuingia kidato cha ....................... katika shule ya Sekondari Kimaghai A kuanzia tarehe ......................... hadi nitakapomaliza kidato cha ..........................

2. Naahidi kuwa, nitatii sheria na kanuni zote za shule na kushiriki katika shughuli zote za shule kikamilifu kulingana na taratibu na ratiba za shule.
3. Tarehe ya kuzaliwa ...................................... Kijiji ............................... Tarafa ......................... Wilaya .............................

**Sahihi ya mwanafunzi .............................................. Tarehe .....................................**

**FOMU NA 02.**

**AHADI YA MZAZI /MLEZI.**

**OFISI YA WAZIRI MKUU**
**TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA**
**HALMASHAURI YA WILAYA YA MPWAPWA**
**SHULE YA SEKONDARI KIMAGHAI A**

PASSPOTI
MZAZI/MLEZI

Mimi (majina kamili) ..........................................................................................namba ya simu .......................................... ninakubali mtoto wangu asome katika shule ya sekondari Kimaghai A kwa muda wote atakaopaswa kuwahapo kimasomo.

1. Jina kamili la baba ...........................................................................................
2. Kazi ya baba .....................................................................................................
3. Jina kamili la mama ...........................................................................................
4. Namba za simu ..................................................................................................
5. Kazi ya mama ....................................................................................................
6. Anuani ya mzazi/mlezi ........................................................................................
7. Wafuatao ni ndugu zake ninaowatambua wanaweza kumsaidia wakati wa dharura,

| | JINA | MAHUSIANO | ANAKOISHI | SIMU |
|---|---|---|---|---|
| i. | ................................ | ................................ | ..................... | .................. |
| ii. | ............................... | ............................... | ....................... | .................. |
| iii. | ............................... | ............................... | ....................... | .................. |
| iv. | ............................... | ............................... | ....................... | .................. |

**PICHA ZA NDUGU WA KARIBU WANNE (4WANAORUHUSIWA KUMTEMBELEA MWANAFUNZI.**

| PICHA YA NO.1 | PICHA YA NO.2 | PICHA YA NO.3 | PICHA YA NO.4 |
|---|---|---|---|

8. Dhehebu la dini ya mtoto ......................................................................................

9. Ripoti za maendeleo ya mwanafunzi ziwe zinatumwa kwa ......................................................................

JINA LA MZAZI /MLEZI ..........................................................................................................
SAINI YA MZAZI/MLEZI .......................................................................................................

FOMU Na. 03

UTHIBITISHO WA DAKTARI

MEDICAL EXAMINATION FORM

To be completed by medical in respect of all form V- VI entrants

Full name ………………………………………. Age ……………………

Sex ……………………………Year …………………

1. Blood count (red and white) ………………………………
2. Urine analysis Test …………………………………………
3. Syphilis Test ……………………………………………………
4. T.B Test ……………………………………………………
5. Eye Test ……………………………………………………
6. Ears ……………………………………………………
7. Spleen ……………………………………………………
8. Abdomen ……………………………………………………

ADDITIONAL INFORMATION
E.g.: Physical defects or impairment (s) Infections Chronic or family diseases etc.

…………………………………………………………………………………………………
…………………………………………………………………………………………………
…………………………………………………………………………………………………
…………………………………………………………………………………………………
…………………………………………………………………………………………………..

……………………………………….. ……………………………….…

NAME AND DESIGNATION SIGNATURE AND OFFICIAL STAMP

……………………………………….. ……………………………….…

STATION DATE

**NOTE.**

Medical officer during the course of this examination, please attend the individual according to any diagnosed case.

This form should be sent tyo school with accceptance form or brought when you come to school. No student is enrolled without certification of physical fitness.